

# Mwongozo wa Kidijitali wa Muwezeshaji

Meta | My Digital World

# Karibu

Mpendwa Muwezeshaji,

Karibu katika **Ulimwengu Wangu wa Kidijitali**, ambayo ni programu ya Meta ya uraia na ustawi wa kidijitali. Ulitengenezwa ili kukusaidia wewe pamoja na wakufunzi wengine huku teknolojia ikiongoza njia tunapoelekea katika mustakabali wa kidijitali.

Wakufunzi kutoka kote duniani wanatambua umuhimu wa kuwafundisha watumiaji wa intaneti kuhusu taarifa, tabia, na ujuzi ambazo huwasaidia watu kustawi katika ulimwengu wa kidijitali unaozidi kuunganika na kuwa changamano. Kuufanyia kazi uraia na ustawi wa kidijitali kunaweza kudumisha usalama wa watu pamoja na kuwawezesha kuleta mabadiliko mazuri katika mazingira yao.

Ulimwengu Wangu wa Kidijitali hukusaidia kuzitambulisha dhana za uraia na ustawi wa kidijitali kwa wanafunzi wako kupitia masomo yaliyotolewa kwa wataalamu wengi ambao ni washirika wetu. Masomo yamejikita katika utafiti wa miaka mingi wa kitaaluma na yanaangazia mitazamo na mambo tofauti ambayo watu kutoka kote duniani wamepitia.

Masomo ya Ulimwengu Wangu wa Kidijitali yamegawika katika nguzo sita za maudhui:

> **Utangulizi wa Mafunzo ya Kidijitali:** Kuwaonesha wanafunzi maana ya intaneti, kutambua taarifa zinazoweza kusambazwa kupitia intaneti, kubaini mbinu tofauti za kupata taarifa mtandaoni na kujua manufaa, majukumu na wajibu wa uraia wa kidijitali.
>
> **Misingi ya Kidijitali:** Kuwafundisha wanafunzi jinsi ya kutumia kikamilifu zana za kulinda vifaa vyao vya kidijitali pamoja na taarifa zao zilizo mtandaoni, pamoja na za watu wengine.
>
> **Ustawi wa Kidijitali:** Kusaidia uwezo wa wanafunzi wa kuamiliana na watu wengine (watu binafsi na umma kwa jumla) mtandaoni katika njia nzuri na zinazojali hisia zao, kulinda afya zao za mwili na akili, na kuchunguza utambulisho wao.
>
> **Kuamiliana Kidijitali:** Kuwasaidia wanafunzi kupata ufahamu, kufikiria kwa makini na ujuzi unaohitajika ili kutathmini na kusambaza taarifa kwenye vyombo vya habari mtandaoni, pamoja na kuamiliana na tamaduni na miktadha mbalimbali.
>
> **Uwezeshaji wa Kidijitali:** Kuwasaidia wanafunzi kutumia teknolojia na mitandao ya kijamii ili kuleta mabadiliko chanya na kutengeneza fursa nzuri zaidi kwa ajili yao wenyewe, jamii zao, na ulimwengu mzima.
>
> **Fursa za Kidijitali:** Kuwatayarisha wanafunzi ili watengeneze mifumo ijayo ya teknolojia na kupata ufanisi katika kazi zao.

Masomo yaliyo katika kila nguzo yamepangwa kwa umakini ili kuwasaidia washiriki wajifunze ujuzi halisi kama vile kulinda taarifa binafsi, kutambua vyanzo vya kuaminika na kutambua mahusiano mazuri ya mtandaoni. Mbali na vifaa vya muwezeshaji, programu ya Ulimwengu Wangu wa Kidijitali inatoa nyenzo na mazoezi ambayo washiriki wanaweza kuyatumia wakiwa nyumbani.

Asante kwa kuwasaidia watumiaji wa intaneti kuwa raia wa kidijitali waliowezeshwa, weledi na wanaojukumika. Tunashukuru kwa fursa ya kushirikiana nawe ili kuboresha upatikanaji wa nyenzo za uraia na ustawi wa kidijitali kwa watu wote, kupitia mpango wa Ulimwengu Wangu wa Kidijitali.

Wako Mwaminifu,

**Antigone Davis**
**Mkuu wa Kimataifa wa Idara ya Usalama, Meta**

# Yaliyomo

KUANZA 4

Utangulizi wa Mafunzo ya Kidijitali 5
Misingi ya Kidijitali 6
Ustawi wa Kidijitali 7
Kuamiliana Kidijitali 8
Uwezeshaji wa Kidijitali 9
Fursa za Kidijitali 10
Faharasa ya Maneno Muhimu 11

MASWALI YANAYOULIZWA MARA KWA MARA 13
KIAMBATANISHO 15

# Kuanza

Programu ya **Ulimwengu Wangu wa Kidijitali** imetengenezwa kuwasaidia watumiaji wa intaneti kupitia mkakati anuwai unaotumia mafundisho rasmi na yasiyo rasmi, pamoja na mazoezi binafsi. Ili kuanza kutumia programu hii, fuata hatua zilizopo hapo chini.

## VIFAA VYA UKAGUZI

Tumia muda kuelewa vifaa vya ufundishaji kabla ya kutoa mafunzo. Programu ya Ulimwengu Wangu wa Kidijitali inajumuisha yafuatayo:

- *Mwongozo wa Muwezeshaji*
- *Taratibu za Mafundisho Zinazopendekezwa*
- *Masomo 34 ya Nguzo Sita (tazama "Kuelewa Muundo wa Somo" hapa chini)*
- *Barua ya Wazazi ya Utambulisho wa Programu(tazama "Kiambatanisho")*

Masomo haya yalitengenezwa ili yaweze kutumika kwa mada na mivuto mbalimbali, muundo wa masomo na ratiba na kufanya iwe rahisi iwezekanavyo kuzijumuisha katika mazingira ya masomo yaliyo na yasiyo rasmi. Ulimwengu wa kidijitali hubadilikabadilika, na pia hivi vifaa vya ufundishaji vimetengenezwa hivyo. Kwa sababu hii, huenda mwongozo huu ukabadilika baada ya muda.

## WAJULISHE WAZAZI

Wajulishe wazazi kwamba unatumia Ulimwengu Wangu wa Kidijitali ili kufundisha kuhusu uraia wa kidijitali na ustawi, na uwaombe wakaboreshe ujuzi huo wakiwa nyumbani. Kwenye tovuti ya Ulimwengu Wangu wa Kidijitali, wazazi watapata vichochezi vya kuanzisha mazungumzo na mazoezi ili kupitia dhana za uraia na ustawi wa kidijitali pamoja na watoto wao.

## FUNDISHA MASOMO

Programu ya Ulimwengu Wangu wa Kidijitali imetengenezwa ili iweze kutolewa kama mtaala kamili au masomo binafsi katika mazingira ya teknolojia ya hali ya juu au chini.

Maelezo ya masomo hayo yameandikwa kikamilifu na yanatoa mwongozo kuhusu jinsi unavyoweza kujiandaa kwa ajili ya masomo hayo na kuyafundisha katika mazingira rasmi na yasiyo rasmi. Masomo hayo yako wazi kiasi kwamba unaweza kuyarekebisha ili yaendane na mahitaji ya wanafunzi wako.

Katika masomo yote, kuna fursa za kurekebisha mifano na majina ili yaendane na mambo ambayo wanafunzi wanafahamu na pia muktadha wa eneo lenu. Fursa hizi zimebainishwa kama "Dondoo za Mwalimu." Tunapendekeza kwamba ulipitie kila somo kabla ya muda wa kulifundisha ili kuhakikisha kwamba mifano iliyotolewa inaendana na muktadha wa eneo la wanafunzi wako.

## KUELEWA MUUNDO WA SOMO

Programu ya Ulimwengu Wangu wa Kidijitali huendesha ujuzi mkubwa wa uraia na ustawi wa kidijitali katika nguzo sita za maudhui: Utangulizi, Misingi, Ustawi, Kuamiliana, Kuwezeshwa, na Fursa. Masomo yaliyo katika kila nguzo yanaweza kufundishwa peke yake au yakifuatana, kuanzia Utangulizi wa Mafunzo ya Kidijitali hadi Fursa za Kidijitali. Maendeleo ya maudhui haya, kama yatafundishwa kwa kufuatana, yanaweza kuwasaidia wanafunzi kutatua masuala ya kawaida katika mtandao hadi wakaweza kutumia ujuzi wao wa kidijitali katika mipango yao ya sasa na ya siku zijazo kuhusu kazi zao.

Ni muhimu kukumbuka kwamba ingawa nguzo hizi na masomo yako yanaweza kufundishwa kwa kufuatana, utaratibu wake unaweza kulingana na umuhimu wa kila ujuzi (tazama "Faharasa") na utategemea muktadha wako au wa wanafunzi wako. Vipengele vya muktadha ambavyo vinaweza kutumika ni pamoja na umri, jinsia, eneo, ustadi, na kiwango cha elimu.

# Utangulizi wa Mafunzo ya Kidijitali

## UTANGULIZI WA MAFUNZO YA KIDIJITALI

Masomo na mazoezi katika sehemu hii yanawasaidia wanafunzi kuelewa intaneti ni nini, kuzifahamu taarifa ambazo zinaweza kusambazwa kupitia intaneti, kujua mbinu tofauti za kupata taarifa mtandaoni na kuyajua manufaa, majukumu na wajibu wa uraia wa kidijitali.

Ujuzi ulioshughulikiwa ni pamoja na mafunzo ya kidijitali pamoja na usalama na ustawi.

| Somo | Mada | Lengo |
|---|---|---|
| 1 | Intaneti ni nini na tunajiungaje? | Wanafunzi watafahamu maana ya intaneti na jinsi ya kuunganishwa nayo. |
| 2 | Taarifa za kidijitali na kusambaza | Washiriki watatambua maana ya taarifa za kidijitali, jinsi zinavyosambazwa kupitia intaneti, na jinsi ya kuzilinda. |
| 3 | Upatikanaji wa taarifa na jamii za mtandaoni | Wanafunzi watabaini mbinu tofauti za kupata taarifa na jamii za mtandaoni kwenye mtandao. |
| 4 | Utambulisho wa kidijitali na sifa ya mtandaoni | Wanafunzi watafahamu manufaa na wajibu unaotokana na kuwa katika jamii ya mtandaoni pamoja na taarifa ambazo ziko wazi kwa umma. |
| 5 | Uraia wa kidijitali na umuhimu wake | Wanafunzi watatambua manufaa, majukumu, na wajibu wa kuwa raia mzuri wa kidijitali. |

## MISINGI YA KIDIJITALI

Masomo na mazoezi ya sehemu hii huwasaidia wanafunzi kuelewa jinsi ya kuunganishwa na kutumia intaneti pamoja na mifumo mingine kwa njia inayofaa. Masomo pia huwasaidia wanafunzi kulinda data na taarifa zao (pamoja na za wengine) na vifaa na rasilimali za kidijitali.

Ujuzi unaoshughulikiwa ni pamoja na upatikanaji wa kidijitali, siri na uelewa wa data.

| Somo | Mada | Lengo |
| --- | --- | --- |
| 1 | Utangulizi wa siri | Washiriki watafikiria kuhusu jinsi wanavyoielewa dhana ya siri yao wenyewe na jinsi inavyoathiri maisha yao binafsi. Washiriki watazingatia aina za taarifa ambazo wangependa ziwe za siri na hali ambazo watasambaza/ hawatasambaza taarifa fulani. |
| 2 | Siri na wewe | Washiriki watachunguza aina za taarifa ambazo zinafaa ziwe za "siri," jinsi ya kubadilisha mipangilio ya usalama katika mitandao ya kijamii na jinsi ya kueleza mchakato wa kufanya maamuzi ya jinsi ya kuweka mipangilio (mfano, kwa nini maudhui mengine yamewekwa kuonwa na "marafiki pekee" bila ya kuonwa na "umma"). |
| 3 | Nywila | Washiriki watajifunza kuhusu jinsi ya kuhakikisha taarifa zao zilizoko mtandaoni ni salama zaidi kwa kutumia na kutunza nywila ngumu. Washiriki watajifunza kuhusu kanuni za kutengneza nywila ngumu na hatari za kusambaza nywila yako. Pia watajifunza kuhusu jinsi ya kutunza vizuri nywila zao na jinsi ya kuchukua hatua za kuzuia akaunti zao zisiingiliwe na watu bila idhini yao. |
| 4 | Miunganisho | Washiriki watajifunza kuhusu mitandao ya Wi-Fi pamoja na manufaa na hatari za kuitumia. Hususani, watajifunza kutambua mitandao isiyolindwa ya Wi-Fi inayopatikana, kuelewa manufaa na hatari za kutumia mitandao isiyolindwa ya Wi-Fi na kufanya maamuzi mazuri kuhusu wakati wa kujiunga na kutumia mitandao isiyolindwa ya Wi-Fi. |
| 5 | Usalama wa mtandaoni, wizi wa mtandaoni na jumbe taka | Washiriki watajifunza kuhusu watu wenye nia mbaya walio mtandaoni wanaoweza kujaribu kutumia udhaifu wa usalama ili kukusanya taarifa zao. Washiriki wataweza kueleza hatari za kuwa mtandaoni, kutengeneza mikakati ya kuwa na tabia salama zaidi, kutambua jumbe taka na kueleza kuhusu nani anayeweza kuomba nywila zao. |

# Ustawi wa Kidijitali

## USTAWI WA KIDIJITALI

Masomo na mazoezi yaliyo katika sehemu hii huwasaidia wanafunzi kuangalia utambulisho wao, kuamiliana na watu wengine (watu binafsi pamoja na makundi ya watu) mtandaoni kwa namna zinazoonesha kujali hisia zao, zinazofuata maadili na namna nzuri na kuzikabili hatari ambazo huenda zikatokana na ulimwengu wa kidijitali ili kulinda afya yao ya mwili na akili.

Ujuzi ulioshughulikiwa ni pamoja na kuangalia na kubuni utambulisho, tabia nzuri/za heshima, na usalama na ustawi.

| Somo | Mada | Lengo |
|---|---|---|
| 1 | Sifa | Washiriki watafikiria kuhusu jinsi taarifa zinazopatikana kwa umma mtandaoni zinavyochangia maoni ya watu wengine kuhusu wao. Watatambua walengwa wa aina tofauti wa mawasiliano ya mtandaoni, kuzingatia ni taarifa gani ambazo wangetaka zionekane wakati mtu anatafuta majina yao na kujifunza njia mbalimbali za kushughulikia maudhui ya mtandaoni yanayowahusu ambayo hawayapendi. |
| 2 | Mitandao ya kijamii na kusambaza | Washiriki watafikiria kuhusu siri huku wakizingatia namna ambavyo wanasambaza taarifa na kuwasiliana na watu wengine mtandaoni, hasa kuhusu matumizi ya mitandao ya kijamii. Wataweza kueleza jinsi ya kuweka uwiano wa hatari na manufaa katika kuweka mipangilio binafsi kwenye mitandao ya kijamii na kujifunza jinsi ya kutumia vizuri mipangilio binafsi ya mtandaoni. |
| 3 | Uwepo katika mtandao | Washiriki wataweza kutambua aina moja ya taarifa binafsi ambayo wanaweza kuisimamia mtandaoni, aina moja ya taarifa ambayo hawawezi kuidhibiti mtandaoni, jambo moja wanaloweza kufanya kuhusu kipengele fulani cha taarifa zao binafsi ambacho hawawezi kudhibiti moja kwa moja. |
| 4 | Mitazamo tofauti | Washiriki watatathmini wajibu wa mitazamo wakati wanatathmini taarifa zinazohusishwa na shughuli na maudhui yao ya mtandaoni au ya wengine. Watapata ufahamu wa vipengele husika vya kimuktadha (mfano, wakati, masuala ya kitamaduni, kijamii, kimtaa/kimkoa/kimataifa) ambayo huathiri shughuli na maudhui ya mtandaoni ya mtu. Aidha, washiriki watazingatia athari za taarifa wanazoweka mtandaoni kuhusu mahusiano yao na jamaa zao, marafiki, walimu, waajiri, na watu wengine. |
| 5 | Unataka Kuwa Nani? | Washiriki watatathmini jinsi utambulisho wao mtandaoni na maudhui wanayotengeneza na kuyasambaza kwa watu wengine yanavyohusiana na malengo yao (mfano, yanayohusiana na kazi, masomo au mambo yanayowavutia maishani ambayo wangependa kujishughulisha nayo). Wataangalia jinsi ya kusimamia utambulisho wa mtandaoni kwa kuzingatia mada, wavuti, jina, mwonekano na mipangilio binafsi. |
| 6 | Muda wangu mimi tu: kipindi cha kujifariji kwa vijana | Washiriki watalinganisha namna ambavyo wanawajibu rafiki zao wa karibu wakati wakiwa na huzuni (na namna wanavyojibiwa) na kuzingatia namna ambavyo wanaweza kujirekebisha wakati wa changamoto. |
| 7 | Wakati ambapo nilihisi kushukuru | Washiriki wataeleza maana ya kushukuru na kutoa mfano wa wakati ambapo walijihisi kushukuru na pia kuelewa kwamba kuna aina nyingi ya mambo yanayoweza kutufanya tujihisi kushukuru. |

# Kuamiliana Kidijitali

## KUAMILIANA KIDIJITALI

Masomo na mazoezi yaliyo katika sehemu hii huwasaidia wanafunzi kufafanua vipengele vya muktadha vinavyotumika (mfano, vya kitamaduni, kijamii, kiwilaya/kimkoa/kimataifa) katika hali fulani na kushiriki ipasavyo katika hali hiyo, pamoja na kupata, kutathmini, kubuni na kusambaza taarifa pamoja na maudhui katika vyombo vya habari tofauti.

Ujuzi ulioshughulikiwa ni pamoja na muktadha, ubora wa taarifa, na uelewa wa vyombo vya habari.

| Somo | Mada | Lengo |
|---|---|---|
| 1 | Heshima na Mipaka | Washiriki watapata uelewa mzuri zaidi wa mitazamo na hisia za wengine katika muktadha wa watu wanaosambaza taarifa binafsi mtandaoni. |
| 2 | Mahusiano Mazuri ya Mtandaoni | Washiriki wataangalia sifa za mahusiano mazuri na yenye utu na jinsi ambavyo tabia za mtandaoni huchangia katika mahusiano mazuri na mabaya. Washiriki pia watatathmini fursa na changamoto zilizomo katika mitandao ya kijamii na mahusiano katika makundi yao na kujifunza jinsi ya kushajiisha tabia miongoni mwa wanakundi wenzao. |
| 3 | Uthibitishaji ni Nini? | Washiriki watajifunza kuhusu maana ya uthibitishaji wa taarifa na kwa nini ni muhimu kwa walengwa wa habari kuthibitisha habari wanazosoma au kutazama. Pia watazingatia wajibu wa mashirika ya habari, walengwa wa habari na makampuni ya mitandao ya kijamii katika kushajiisha mazingira ya usambazaji wa taarifa za kweli. |
| 4 | Hatua za Uthibitishaji | Washiriki watajifunza kuhusu orodha ya ukaguzi ya hatua 5 wanayoweza kutumia kuthibitisha asili, chanzo, tarehe, eneo na nia ya picha au video. Watatambua matatizo yaliyo katika mchakato wa uthibitishaji na kuanza kufikiria kuhusu zana mbalimbali za mtandaoni na zisizo za mtandaoni wanazoweza kutumia ili kuchunguza uhalisia wa maudhui ya mtandaoni. Washiriki watatafakari kuhusu jinsi nia ya chanzo cha taarifa inavyoweza kuathiri namna ambavyo kisa fulani kitaonekana. |
| 5 | Aina za Matini za Vyombo vya Habari | Washiriki wataweza kueleza maana ya nakala (iliyonakiliwa kutoka kwa nakala ya asili) na kueleza kwa nini kuongezeka kwa kasi kwa machapisho yenye maandishi kunaweza kufanya mchakato wa uthibitishaji kuwa mgumu zaidi wakati wa habari za hivi punde. Watatengeneza na kusambaza nakala zao za maudhui mtandaoni huku wakifikiria kuhusu wakati ambapo ni muhimu kutambua chanzo cha nakala au muktadha wa asili wa habari za kisa fulani. |
| 6 | Mtu mwema zaidi unayeweza kuwa | Washiriki watafikiria na kuandika kuhusu maisha yao wakiwa na miaka 40. |

## UWEZESHAJI WA KIDIJITALI

Masomo na mazoezi ya sehemu hii huwasaidia wanafunzi kushiriki katika masuala ya umma, kupigania masuala wanayojali, kutengeneza maudhui, na kuelewa na kutumia dhana za kisheria.

Ujuzi unaoshughulikiwa ni pamoja na maamiliano ya kiraia na kisiasa, utengenezaji wa maudhui na sheria.

| Somo | Mada | Lengo |
|---|---|---|
| 1 | Utetezi na kuleta mabadiliko | Washiriki watajifunza kuhusu dhana ya utetezi kwa kutambua tatizo linaloathiri jamii yao na kisha kufikiria mabadiliko mawili ambayo wangependa kuona katika siku zijazo kuhusu tatizo hilo. |
| 2 | Kutengeneza mtandao wako wa utetezi | Washiriki watajifunza jinsi mitandao ya watu inavyoweza kutumika vyema ili kushajiisha jitihada za utetezi. Washiriki pia watajifunza jinsi ya kutengneza maudhui ya mtandaoni ili kueneza taarifa kuhusu lengo wanalotaka kutekeleza. |
| 3 | Uhamasishaji kupitia vyombo vya habari | Washiriki watajifunza kuhusu, na kutambua njia ambazo aina tofauti za vyombo vya habari zinaweza kutumiwa ili kushajiisha watu kuhusu suala fulani. |
| 4 | Alama za Reli | Washiriki watajifunza jinsi ambavyo alama za reli zimetumika vizuri katika kushajiisha kampeni za kupigania masuala ya kijamii. Washiriki pia watafahamu jinsi ambavyo alama za reli katika mitandao ya kijamii zinaweza kusaidia kuhamasisha watu kuhusu suala la utetezi na watabuni alama zao za reli na mbinu za kukuza uhamasishaji kuhusu masuala yaliyo muhimu kwao. |
| 5 | Ni wakati wa kuchukua hatua! | Washiriki watajifunza jinsi ya kutengeneza mpango wa awali wa kampeni zao wenyewe za utetezi. |
| 6 | Kuangalia maadili yako binafsi | Washiriki wataainisha orodha ya maadili kulingana na umuhimu wa maadili hayo na kutafakari kuhusu jinsi maadili muhimu zaidi yanavyoathiri maisha yao pamoja na mipango yao ya siku zijazo. |

# Fursa za Kidijitali

## FURSA ZA KIDIJITALI

Masomo na mazoezi ya sehemu hii huwasaidia wanafunzi kujifunza ujuzi wanaohitaji ili kuzitumia kikamilifu fursa zinazotolewa na ulimwengu wa kidijitali. Hii ni pamoja na uwezo wa kuelewa na kushiriki katika mazungumzo kuhusu akili bandia, kuelewa na kutumia dhana za ukokotoaji, kushiriki katika kutengeneza, kukusanya, kufafanua na kuchanganua data na kuendesha shughuli za kiuchumi ndani na nje ya mtandao.

Ujuzi ulioshughulikiwa ni pamoja na akili bandia, kusahilisha matatizo ya kompyuta, data, na uchumi wa kidijitali.

| Somo | Mada | Lengo |
|---|---|---|
| 1 | Kuangalia Mambo Tuliyopitia | Washiriki watajifunza jinsi ya kutambua matukio mahususi ambayo yamechangia kuwatengeneza watu walivyo hivi sasa, kutafakari kuhusu jinsi matukio kama hayo yanavyoweza kuwa na umuhimu mkubwa kwa mustakabali wao na kufikiria kuhusu njia wanazoweza kutumia kupitia matukio mapya yatakayowasaidia kutimiza malengo yao. |
| 2 | Kutambua Uwezo Wetu | Washiriki watatambua aina tatu za ujuzi walio nao — ujuzi unaoweza kutumika katika nyanja mbalimbali, elimu/maarifa, na ujuzi tabia binafsii — na wafikirie jinsi wanavyoweza kutumia ujuzi huo kwa pamoja na kuutumia katika shughuli za siku zijazo. |
| 3 | Kutengeneza Wasifu | Washiriki watajifunza kuhusu mitindo tofauti ya wasifu na kufanya mazoezi ya kuandika wasifu wakizingatia mambo wanayopendelea, mambo waliyopitia, ujuzi na malengo. Washiriki pia watajifunza kuhusu maana ya wasifu na kwa nini ni muhimu katika kufanikisha malengo ya muda mrefu. |
| 4 | Algorithimu ni Nini? | Washiriki wataelewa maana ya algorithimu, umuhimu wa algorithimu, na jinsi algorithimu inavyotumika katika maisha ya kila siku na pia katika sayansi ya kompyuta. |
| 5 | Mitandao ya Kijamii na Algorithimu | Washiriki wataweza kuelewa njia mbalimbali ambazo algorithimu husaidia kubaini maudhui wanayoona katika mitandao ya kijamii na kutumia uelewa huo katika milisho yao ya mitandao ya kijamii. |

# Faharasa ya Maneno Muhimu

**KIFAA CHA MUUNGANISHO:** Hiki ni kifaa chochote kinachosambaza mawimbi ya Wi-Fi na kuwezesha upatikanaji wa Intaneti.

**AKILI BANDIA:** Uwezo wa kuelewa algorithimu zinazotumika katika mifumo ya akili bandia ambayo mtu huingiliana nayo pamoja na mazungumzo ya kimaadili kuhusu ukuzaji wa teknolojia hizi.

**KUSHIRIKI KATIKA SHUGHULI ZA KIRAIA NA KISIASA:** Uwezo wa kushiriki katika masuala ya kiraia (mfano, haki za jamii ya LGBTQ, kuleta amani, kushughulikia hotuba za chuki) na kupigania mambo ambayo mtu anajali — kutumia zana zilizo na zisizo za kidijitali — ili kuboresha hali ya maisha ya mtu katika jamii kutoka katika viwango vya chini hadi vya juu vya uchumi (Levine, 2007).

**KUSAHILISHA MATATIZO YA KOMPYUTA:** Uwezo wa kuelewa na kutumia dhana, taratibu na mitazamo katika matumizi ya kompyuta. Dhana katika matumizi ya kompyuta ni pamoja na dhana ambazo watu hutumia wanapotengeneza programu (mfano, kutambua msururu wa hatua za shughuli fulani, au kuendesha misururu mara nyingi inayofanana). Taratibu katika matumizi ya kompyuta ni zile ambazo watu hupata huku wakitengeneza programu (mfano, kufanya majaribio na kurudiarudia maagizo, kutumia upya na kuchanganya, au kutengneza kitu fulani kwa kutumia mawazo au kazi ambazo tayari zipo). Mwisho, mitazamo katika matumizi ya kompyuta ni mitazamo ambayo watu hutengeneza kuhusu wao, mahusiano yao na watu wengine (kama katika jamii za mtandaoni zenye ushirikiano), na ulimwengu wa teknolojia kwa jumla (mfano, kuelewa uwezo unaotokana na kutengeneza maudhui pamoja na watu wengine na kwa ajili ya watu wengine) (Brennan & Resnick, 2012).

**KUTENGENEZA MAUDHUI:** Uwezo wa kutengeneza maudhui (ya kidijitali) kwa kutumia zana (za kidijitali).

**MUKTADHA:** Uwezo wa kufahamu, kuelewa na kufafanua vipengele vinavyotumika katika muktadha fulani (kwa mfano, kitamaduni, kijamii, kiwilaya/kimkoa/kimataifa) katika hali fulani — huku mkazo ukitiliwa kwa mambo ambayo watu kutoka makundi yenye uwakilishi mdogo wamepitia pamoja na mitazamo yao, haijalishi kama yanahusiana na umri, kabila, rangi, jinsia na mwegemeo wa kijinsia, dini, taifa la asili, eneo, kiwango cha ujuzi au elimu, na/au hali ya masuala ya kijamii na kiuchumi — na kuweza kushiriki kikamilifu katika hali hiyo.

**DATA:** Uwezo wa kufahamu, kuunda, kukusanya, kuwakilisha, kutathmini, kutafsiri na kuchanganua data kutoka kwenye vyanzo vya kidijitali na visivyo vya kidijitali.

**UPATIKANAJI WA KIDIJITALI:** Uwezo wa kuunganisha na kuipata intaneti, kwa mtu binafsi au watu wengi (mfano, teknolojia zinazounganisha watumiaji wengi).

**UCHUMI WA KIDIJITALI:** Uwezo wa kutekeleza shughuli za kiuchumi ndani na nje ya mtandao ili kuchuma rasilimali za aina tofauti za kiuchumi, kijamii, na/au kitamaduni (mfano, kupata pesa, kuongeza mitandao ya watu, kutengeneza jina binafsi).

**UELEWA WA MASUALA YA KIDIJITALI:** Uwezo wa kutumia intaneti pamoja na zana na mifumo mingine ya kidijitali ili kupata, kuingiliana, kutathmini, kutengeneza na kutumia taarifa upya kwa njia nzuri (Palfrey & Gasser, 2016). Uwezo wa kuelewa na kutatua matatizo katika dhana za kidijitali (Carretero, Vuorikari & Punie, 2017).

**KUANGALIA NA KUBUNI UTAMBULISHO:** Uwezo wa kutumia zana (za kidijitali) ili kuchunguza vipengele vya utambulisho wa mtu, na kuelewa jinsi jamii inavyochangia kutengeneza utambulisho wa mtu.

# Faharasa ya Maneno Muhimu

**UBORA WA TAARIFA:** Uwezo wa kupata,kuingiliana, kutathmini, kubuni, na kutumia taarifa upya (kwa jumla; mfano; habari, taarifa za afya, taarifa binafsi) kwa namna nzuri (Palfrey & Gasser, 2016).

**INTANETI:** Mtandao mkubwa wa kompyuta unaounganisha mitandao midogo ya kompyuta kote ulimwenguni. Intaneti ina mitandao ya biashara, elimu, serikali, na mitandao mingine.

**SHERIA:** Uwezo wa kuamiliana na mifumo, dhana, na mawazo ya kisheria kuhusu intaneti na zana zingine za kidijitali (mfano, haki za kunakili, matumizi yenye usawa) na uwezo wa kutumia mifumo hii katika shughuli zako.

**UELEWA WA VYOMBO VYA HABARI:** Uwezo wa kuchanganua, kutathmini, kusambaza na kutengeneza maudhui ya muundo wowote wa vyombo vya habari (mfano, yaliyochapishwa, ya kutazama, yanayoshirikisha watumiaji, ya sauti) na kushirikisha katika jamii na mitandao. Uelewa wa vyombo vya habari (Hobbs, 2010), unajumuisha mambo ambayo watafiti wengine wanachukulia kuwa "uelewa mpya" (Lankshear & Knobel, 2007), na "uelewa mpya wa vyombo vya habari" (Jenkins, Clinton, Purushotma, Robison & Weigel, 2006). Yaani, zinajumuisha mitazamo ya uelewa ambayo haijikiti tu katika kuamiliana kwa watu na vyombo vya habari (uelewa wa vyombo vya habari) ila pia una stadi zinazoangazia uhusishwaji wa jamii na desturi za ushirikishaji. "Uelewa wa vyombo vya habari" pia unajumuisha ufahamu wa kusoma na kuandika.

**MODEMU:** Modemu ni kifaa kinachotengeneza na kudumisha muunganisho kwa Mtoa Huduma za Intaneti (ISP) wako ili kukuwezesha kupata intaneti. Modemu hubadilisha mawimbi kutoka nje ya eneo lako mahususi kuwa mawimbi yanayoweza kusomwa na kompyuta yako pamoja na vifaa vingine vya kidijitali.

**MTANDAO:** Mtandao ni mkusanyiko wa mifumo ya kompyuta na vifaa vilivyounganishwa pamoja kutoka kote ulimwenguni.

**TABIA NZURI/ZA HESHIMA:** Uwezo wa kuingiliana na watu wengine (watu binafsi pamoja na umma kwa jumla) mtandaoni kwa namna yenye heshima, maadili mema, uwajibikaji wa kijamii na kuelewa hisia za wengine.

**SIRI NA SIFA:** Uwezo wa kulinda taarifa zako binafsi na za wengine katika mtandao. Ufahamu wa "alama" za kidijitali zinazoachwa baada ya shughuli ambazo mtu hufanya mtandaoni, matokeo ya muda mfupi na mrefu ya alama hizi, jinsi ya kusimamia alama za mtandaoni ipasavyo, pamoja na kuwa na ufahamu kuhusu data zilizotokana na taarifa zingine (yaani, data mpya zilizopatikana kwa kunasa na kuchanganua data zingine, ambazo huenda zikatoa maelezo mapya kuhusu mtu (van der Hof, 2016)).

**RUTA:** Ruta ni kifaa ambacho hutengeneza mtandao kati ya vifaa vyote (mfano kompyuta, vishikwambi, simu za mkononi) katika eneo fulani (kama vile shule, maktaba au nyumbani kwako).

**USALAMA NA USTAWI:** Uwezo wa kuzikabili hatari ambazo huenda zikaletwa na ulimwengu wa kidijitali ili kulinda afya yako ya mwili na akili (mfano kujilinda dhidi ya uraibu wa intaneti na majeraha yanayotokana na matumizi ya viungo kupita kiasi). Hatari za mtandaoni zinaweza kuwekwa katika kategoria kubwa tatu: matendo (unyanyasaji wa mtandaoni, unyanyasaji wa kimapenzi au kutumia mtu jumbe za kingono ambazo hataki), mawasiliano (mfano, kukutana ana kwa ana baada ya kuwasiliana mtandaoni, kuwasiliana na watu wanaojifanya mtu mwingine), na maudhui (mfano, kutazama ponografia, maudhui yenye vurugu au ghasia, maneno ya chuki, maudhui kuhusu dawa za kulevya, maudhui ya ubaguzi wa rangi) (Livingstone, Kirwall, Ponte & Staksrud, 2013).

**USALAMA:** Uwezo wa kulinda taarifa binafsi, vifaa vya kidijitali na rasilimali zako (mfano, taarifa za kuingia kama vile nywila, wasifu, na tovuti).

# Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara

## ULIMWENGU WANGU WA KIDIJITALI HUKUPA NINI KINGINE?

Mbali na moduli sita za mafunzo zilizo kwenye tovuti, programu ya Ulimwengu Wangu wa Kidijitali pia inatoa miongozo kwa wakufunzi kuhusu taratibu zinazopendekezwa za kufundisha wanafunzi ndani na nje ya mtandao na kutoa nyenzo kwa wazazi na walezi za kutumia nyumbani ili kutilia mkazo masomo yaliyofundishiwa darasani.

## MASOMO HAYA YAMETENGENEZWA KWA AJILI YA NANI NA YALITENGENEZWA VIPI?

Masomo haya yametengenezwa kwa ajili ya wanafunzi wenye miaka 13-18 walio Kusini mwa Jangwa la Sahara. Mtaala huu umetengenezwa huku ukiwa na maelekezo ya hatua kwa hatua kwa ajili ya walimu wa wanafunzi wenye umri huo. Masomo haya yametolewa katika nyenzo za wataalamu mbalimbali ambao ni washirika, wenye tajriba katika kutengeneza maudhui na mitaala. Tafadhali angalia ukurasa wa Kuhusu Sisi kwenye tovuti ili kujifunza zaidi kuhusu washirika wetu wa maudhui.

## SOMO LINAKUWAJE?

Kila somo limeandikwa kikamilifu lakini linawapa wakufunzi fursa ya kurekebisha maudhui ili yaendane na mahitaji ya wanafunzi wao mahususi. Masomo haya hutumika katika jamii zenye teknolojia za hali ya juu na chini — masomo mengi yametengenezwa kwa ajili ya mazingira ya masomo yenye ufikiaji mdogo wa intaneti au yasiyo na intaneti.

## JE, MASOMO HAYA YANAWEZA KUTUMIKA KATIKA MAFUNDISHO YA MTANDAONI?

Ndiyo, masomo haya yametengenzwa ili kutumika katika mafundisho ya ana kwa ana na ya mtandaoni, huku wawezeshaji wanaofundisha mtandaoni wakipewa maelekezo maalum.

## JE, UNAWEZA KUNIPA MFANO WA JINSI NINAVYOWEZA KUJUMUISHA SOMO FULANI KATIKA DARASA LANGU?

Masomo yanaweza kujumuishwa katika mtaala mzima wa shule. Hii hapa ni mifano michache ya masomo matano yafuatayo: Historia, Kiingereza, Sayansi, Hisabati na Lugha ya Kimataifa.

### HISTORIA

Kushiriki Katika Shughuli za Kiraia na Kisiasa: Linganisha vuguvugu la kihistoria lililoangazia suala la jamii na vuguvugu la hivi karibuni. Je, watu waliwasiliana vipi baina yao katika vuguvugu hilo? Je, mavuguvugu hayo yaliangaziwa vipi katika vyombo vya habari? Kama sehemu ya zoezi hili, unaweza kutambulisha somo la "Alama za Reli" kwa wanafunzi.

# Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara

## KIINGEREZA

Usalama: Waombe wanafunzi waandike insha zenye ushawishi kuhusu mada inayohusiana na usalama. Mfano unaweza kujumuisha wanafunzi wanaounga mkono au kupinga kuunganisha vifaa binafsi kwenye mtandao wa Wi-Fi wa shule. Katika mchakato huo, huenda wanafunzi wakakutana na wajuzi. Mojawapo ya malengo yao ni kuhakikisha taarifa hizo zinaeleweka kwa ujumla kwa umma. Kama sehemu ya zoezi hili, unaweza kutambulisha somo la "Wi-Fi ya Umma" kwa wanafunzi.

Kuangalia na Kubuni Utambulisho: Waombe wanafunzi watengeneze wasifu katika mitandao ya kijamii (halisi au wa uongo) kwa ajili ya watu wanaozungumziwa katika maandishi yanayosomwa na darasa. Waombe wanafunzi wachague picha ya wasifu, jina la mtumiaji, sehemu ya "Kuhusu Mimi", orodha ya marafiki, na machapisho na/au picha chache ambazo huenda mtu huyo anaweza kuzisambaza. Omba wanafunzi wazingatie machapisho ambayo mtu huyo huyasambaza kwa umma, na mambo ambayo wewe msomaji unayafahamu tu kwa sababu ya uchanganuzi wa msimulizi. Unaweza kuomba wanafunzi tofauti watengeneze wasifu kwa ajili ya mtu huyo mmoja kisha uombe darasa lilinganishe kila moja ya wasifu zilizotengenezwa. Je, kwa nini wanafunzi walifanya maamuzi kuhusu maudhui ambayo wangeweka katika wasifu walizotengeneza? Je, kila wasifu unawakilisha vizuri mambo tunayofahamu kutokana na maandishi? Kwa nini au kwa nini siyo? Kama sehemu ya zoezi hili, unaweza kutambulisha kwa wanafunzi somo la "Uwepo Katika Mtandao".

## SAYANSI

Uchumi wa Kidijitali: Vyombo vya habari vya mtandaoni zinazofundisha watu kuhusu dhana za kisayansi namna zilivyokuwa maarufu, huku wanaoendesha vituo vya YouTube, mabloga na watu kama vile Bill Nye na Neil deGrasse wote wakitumia zana za mawasiliano za kidijitali ili kutengeneza jina mtandaoni inayofanya dhana changamano za kisayansi ziweze kufikiwa na watu wengi. Pamoja na wanafunzi wako, tambua jinsi watu hawa maarufu wanaotengeneza maudhui ya sayansi katika mtandao wanapata imani kwa watu wanaotazama/kusoma maudhui yao, jinsi wanavyodondoa taarifa za kisayansi na mikakati tofauti wanayotumia ili kuhakikisha maudhui yao yanaburudisha watu wanaoyatazama. Jadili ujuzi ambao wanafunzi wanadhani unatumika katika utengenezaji wa maudhui haya (mfano, utafiti, fikira bunifu, utengenezaji wa vyombo vya habari). Kwa kufuata taratibu hizi zinazopendekezwa, waombe wanafunzi wako watengeneze maudhui kwa ajili ya kituo maarufu cha sayansi cha YouTube, ukurasa wa tovuti au blogu na wafikirie kuhusu baadhi ya stadi ambazo wamepata kupitia mchakato huu. Jadili tofauti zilizopo katika kuandaa maudhui kwa ajili ya wataalamu wa sayansi dhidi ya umma wa kawaida. Kama sehemu ya zoezi hili, unaweza kutambulisha somo la "Kutambua Uwezo Wetu" kwa wanafunzi.

## HISABATI

Ubora wa Taarifa: Tambua kisa kinachoonesha dhana fulani ya hesabu kwa namna isiyokuwa wazi. Mfano mzuri ni takwimu inayopotosha. Waombe washiriki wachunguze chanzo cha takwimu hiyo (mfano, takwimu hii imetoka kwenye makala gani ya utafiti?). Je, wanaona takwimu hizo katika visa vingine vya habari? Kama ndiyo, wahimize wanafunzi watengeneze mlisho wa vyanzo ambapo takwimu hiyo ilionekana. Jadili: Kwa kila chanzo, je, matumizi ya takwimu hiyo huenda yalisababishwa na nini? Kuna athari gani (halisi au ambayo huenda ikatokea) ya kuweka takwimu ya aina hii kwenye kisa/visa? Kama sehemu ya zoezi hili, unaweza kutambulisha somo la "Zaidi ya Suala la Asili" kwa wanafunzi.

## LUGHA YA KIMATAIFA

Kushiriki Katika Shughuli za Kiraia na Kisiasa: Waombe wanafunzi wachague suala la utetezi ambalo wana ari nalo. Wahimize watafute picha zenye matini zinazoangazia suala hili, zilizo katika lugha lengwa. Jadili na wanafunzi: Ni taratibu zipi zinazotumika ambazo ziko sawa au tofauti na desturi za picha zenye matini zinazotumika katika muktadha wa eneo lako? Je, picha hizo ndizo zilizotumiwa kutengeneza picha zenye matini katika lugha lengwa? Kulingana na taratibu walizoona, wahimize watengeneze picha zao zenye matini katika lugha lengwa na watoe mawazo kuhusu jinsi wanavyoweza kueneza jumbe za vyombo vya habari za mtandaoni ili kuhamasisha watu kuhusu jitihada wanayotekeleza. Kama sehemu ya zoezi hili, unaweza kutambulisha somo la "Kufanya Uhamasishaji Kupitia Vyombo vya Habari" kwa wanafunzi.

# Kiambatanisho

## BARUA YA MZAZI

**Mpendwa Mzazi au Mlezi,**

Natumai kwamba uko salama. Ningependa kutumia muda kukueleza kuhusu uraia na ustawi wa kidijitali. Tutajifunza kuhusu mada hii katika muda wa wiki chache zijazo tukitumia vifaa kutoka katika programu ya Meta ya Ulimwengu Wangu wa Kidijitali. Masomo yamejikita katika utafiti wa kitaaluma na yanaangazia mitazamo na mambo tofauti ambayo watu wachanga kutoka kote duniani wamepitia.

Uraia na ustawi wa kidijitali ni taarifa, tabia na ujuzi ambao hutusaidia kutumia intaneti na zana zingine za kidijitali kwa njia salama. Hii ni pamoja na hatua tunazozichukua ili kujilinda, kama vile kutumia mipangilio binafsi ili kulinda taarifa binafsi. Pia inajumuisha kufanya maamuzi mazuri na kuwasliana na watu wengine mtandaoni.

Kuelewa uraia na ustawi wa kidijitali kunaweza kuwasaidia watoto wote kupata ufanisi katika ulimwengu wa kidijitali unaozidi kuunganika na kuwa changamano. Kunaweza kudumisha usalama wao huku kukiwawezesha kuleta mabadiliko mazuri katika jamii zao. Kwa sababu ya umuhimu wa uraia na ustawi wa kidijitali kwa watoto wetu, ningependa kukualika ili pia nawe uhusike katika programu hii.

Programu ya Ulimwengu Wangu wa Kidijitali ina nyenzo za wazazi ambazo unaweza kutumia ili kumsaidia mtoto wako ajifunze zaidi kuhusu uraia wa kidijitali na ustawi. Tunakuhimiza ujifunze zaidi kuhusu nguzo sita za maudhui ya uraia wa kidijitali na ustawi zilizo hapa chini:

**Utangulizi wa Mafunzo ya Kidijitali:** Kuwaonesha wanafunzi maana ya intaneti, kutambua taarifa zinazoweza kusambazwa kupitia intaneti, kubaini mbinu tofauti za kupata taarifa mtandaoni, na kugundua manufaa, majukumu, na wajibu wa uraia wa kidijitali.

**Misingi ya Kidijitali:** Kuwafundisha wanafunzi jinsi ya kutumia kikamilifu zana za kulinda vifaa vyao vya kidijitali pamoja na taarifa zao zilizo mtandaoni, pamoja na za watu wengine.

**Ustawi wa Kidijitali:** Kusaidia uwezo wa wanafunzi wa kuamiliana na watu wengine (watu binafsi na umma kwa jumla) mtandaoni katika njia nzuri na zinazojali hisia zao, kulinda afya zao za mwili na akili, na kuchunguza utambulisho wao.

**Kuamiliana Kidijitali** Kuwasaidia wanafunzi kupata stadi za ufahamu, kufikiria kwa makini na ujuzi unaohitajika ili kutathmini na kusambaza taarifa kupitia vyombo vya habari vya mtandaoni, pamoja na kuingiliana na tamaduni na miktadha mbalimbali.

**Uwezeshaji wa Kidijitali:** Kuwasaidia wanafunzi kutumia teknolojia na mitandao ya kijamii ili kuleta mabadiliko chanya na kujenga fursa nzuri zaidi kwa ajili yao wenyewe, jamii zao, na ulimwengu mzima.

**Fursa za Kidijitali:** Kuwatayarisha wanafunzi ili watengeneze mifumo ijayo ya teknolojia na wapate ufanisi katika kazi zao.

Unaweza kutumia vichochezi vya kuanzisha mazungumzo na mazoezi katika sehemu ya wazazi kwenye tovuti ili kupitia dhana za uraia na ustawi wa kidijitali pamoja na mtoto wako. Unaweza kuzipata nyenzo hizi hapa mydigitalworld.fb.com/learning/ssa/.

Ujuzi wa uraia na ustawi wa kidijitali ni muhimu na unahitajika kwa mustakabali wa watoto wetu. Ninakusudia kushirikiana na mtoto wako anapojifunza kutumia intaneti kwa namna salama na kwa kuwajibika na kupata ufanisi katika ulimwengu wa kidijitali.

Asante kwa usaidizi wako tunapoangalia mada hii mpya. Ikiwa una maswali yoyote, tafadhali wasiliana nami.